

HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri S.L.P 88-Kwimba

SIMU: 0732-980 832
FAX: 0732-980 832



S.L.P 88,
KWIMBA.

Kumb. Na MZA/KDC/M70/30/112

Tarehe: 3/5/2018

TANGAZO LA KAZI

WAUGUZI WAKUNGA (EN): 9
TABIBU CO/RN: 5
WATEKNOLOJIA MAABARA: 3

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri wa Wilaya ya Kwimba kwa niaba ya mdau/shirika lisilo la kiserikali la AGPAHI anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa za kuomba nafasi za wauguzi, matabibu au wauguzi waliosajiliwa na wataalamu wa maabara kwa ajira ya masharti ya mkataba (contract) kama ifuatavyo;

SIFA ZA MWOMBAJI

MUUGUZI MKUNGA (EN/RN)

- Mwombaji awe na elimu ya kidato cha nne au cha sita na amehitimu mafunzo ya uuguzi na ukunga kwa ngazi ya cheti kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali

KAZI NA MAJUKUMU

- 1) Kufanya kazi za kiuguzi na kuhudumia wateja katika jamii, hospitalini na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya
- 2) Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi
- 3) Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa ya utendaji wake wa kazi
- 4) Kutoa huduma za afya kwa wagonjwa majumbani
- 5) Kutoa ushauri nasaha

- 6) Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
- 7) Kutoa huduma za uzazi na afya ya mtoto
- 8) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
- 9) Kufuatilia na kutunza vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi

TABIBU (CLINICAL OFFICER)

- Mwombaji awe na elimu ya kidato cha nne au cha sita na amehitimu mafunzo ya utabibu kwa ngazi ya diploma kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali.

KAZI/MAJUKUMU

- 1) Kufanya kazi zote za tabibu msaidizi
- 2) Kutambua na kutibu magonjwa ya kawaida
- 3) Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake
- 4) Kufanya upasuaji mdogo
- 5) Kushiriki katika kupanga na kutekeleza huduma za afya msingi
- 6) Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za afya za mfuko wa afya ya jamii
- 7) Kuweka kumbukumbu ya vifaa na zana za kutolea huduma
- 8) Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji

MTEKNOLOJIA MAABARA (LAB TECHNOLOGIST)

- Mwombaji awe na elimu ya kidato cha nne au cha sita na amehitimu mafunzo ya utabibu kwa ngazi ya diploma kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali.

KAZI/MAJUKUMU

- 1) Kupima sampuli zinazoletwa maabara
- 2) Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa maabara ngazi za juu
- 3) Kufanya kazi ya ukaguzi wa maabara, vitendanishi, vifaa, kemikali, na hifadhi ya kemikali.
- 4) Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi
- 5) Kufundisha watumishi walio chini yake

MSHAHARA:

MUUGUZI: kuanzia TGHS A

TABIBU: kuanzia TGHS B

MTEKNOLOJIA MAABARA: kuanzia TGHS B

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- 1) Muombaji awe raia wa Tanzania
- 2) Muombaji awe hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai
- 3) Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu na cheti cha kuzaliwa
- 4) Results slip, provisional results na statement of results **havitakubalika**
- 5) Maombi ya yaambatanishwe na picha mbili za passport size za hivi karibuni
- 6) Maombi yaambatanishwe na wasifu (CV) zenye mawasiliano ya uhakika
- 7) Muombaji awe na umri unaoanzia miaka 18 na usiozidi 45.
- 8) Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na cha sita waliosomea nje ya nchi wahakikishe vyeti vimehakikiwa na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (NACTE)


Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **18/5/2018 saa 9:30 alasiri**.

Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa kutumia anuani ifuatayo:

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 88,
NGUDU-KWIMBA.**

Tangazo hili pia linapatikana kwenye mbao za matangazo na katika tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ambayo ni: www.kwimbadc.go.tz

Imetolewa na;


STAMILI A. NDARO

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA KWIMBA

*MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA*